

MBOLEA BORA KWA KILIMO ENDELEU

Mbolea YETU

Tanzania

ISSN 2799-2039

Toleo Na. 04 - Julai - Desemba 2022

Rais Samia: Simamieni vema Mpango wa ruzuku ya mbolea



WIZARA YA KILIMO
MAMLAKA YA UDHIBITI WA MBOLEA TANZANIA (TFRA)



Matumizi ya mbolea katika mazao ya mizizi – **Uk.5**



Maadhimisho Siku ya Mbolea Duniani 2022 – **Uk.11**

UJUMBE WA MKURUGENZI MTENDAJI

Mantiki ya ruzuku ya mbolea ni kuimarisha usalama wa chakula, kuongeza malighafi viwandani



Dkt. Stephan Eliuth Ngailo
Mkurugenzi Mtendaji

NI jambo la faraja kwamba serikali yetu kwa mwaka 2022/2023 ime-tenga shilingi bilioni 150 kugharamia ruzuku ya mbolea kwa wakulima nchi-ni ili kupunguza makali ya bei ya bidhaa hiyo, kuongeza uzalishaji na tija katika kilimo, kuimarisha usalama wa chakula na kuongeza upatikanaji wa malighafi za viwanda vya ndani.

Hatua hii ya kishujaa ya serikali imetokana na kupanda kwa bei za mbolea hapa nchini na kwenye soko la dunia. Utoaji wa ruzuku umezingatia mahitaji halisi ya mkulima wa Tanzania kulingana na taarifa za usajili na Bajeti ya Serikali.

Mbolea zilizohusika kwenye ruzuku ni zile za kupandia na kukuzia -- DAP na Urea. Mbolea hizi ni takribani asilimia 50 ya matumizi yote ya mbolea nchini. Mbolea za kupandia na kukuzia za aina nyingine zimehusishwa kwenye ruzuku kulingana na mahitaji ya soko. Katika kuhamasisha matumizi ya mbolea zinazozalishwa nchini, mbolea zetu zinazozalishwa na viwanda vya ndani zimeingia kwenye mpango wa ruzuku kutokana na mahitaji ya soko.

Ni kutokana na uzoefu uliopatikana wa utekelezaji wa mipango ya ruzuku katika miaka iliyopita, ndiyo maana serikali imeamua kutumia mfumo wa kidijitali kutekeleza mpango wa ruzuku ya mbolea itakayotolewa kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023.

Lengo ni kuongeza ufanisi wa utoaji wa ruzuku, kupunguza mianya ya udanganyifu, rushwa, na muda na gharama za usimamizi.

Mfumo huu umetumia programu maalum ya kidijitali, au kwa Kiingereza, Digital Platform, kuratibu shughuli zote za utekelezaji ruzuku kuanzia utambuzi wa washiriki wa mfumo wakiwemo waingizaji na wazalishaji wa mbolea, wafanyabiashara, wakulima na aina za mbolea zitakazokuwa katika mpango wa ruzuku; kuratibu usambazaji; uuzaji wa mbolea kwa wakulima; na malipo ya ruzuku ya mbolea.

Mfumo huu ulibuniwa kufanya kazi kama ifuatavyo:

* Makampuni yataingiza/yatazalisha mbolea nchini na kuifungasha katika mfuko yenye uzito wa kilo 25 na 50 ambayo imeandikwa "MBOLEAYA RUZUKU" na imechapwa QR code iliyotolewa na Mamlaka ya Udhhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA);

* Makampuni yatasambaza mbolea kwenye vituo vya mauzo na mawakala na zoezi hilo litahusisha utoaji na upokeaji wa mzigo kwenye mfumo kati ya kampuni na kituo cha mauzo au wakala;

* Mkulima aliyesajiliwa ataenda kwa mfanyabiashara wa mbolea aliyesajiliwa kwa ajili ya kununua mbolea na kuonyesha namba ya utambulisho aliyopewa wakati wa usajili;

* Mfanyabiashara ataingiza namba ya utambulisho wa mkulima kwenye mfumo na kuhakiki taarifa zake kabla ya kumuuzia mbolea;

* Mkulima atafanya malipo ya mbolea kwa mfanyabiashara kwa bei elekezi ya ruzuku iliyowekwa;

* Wakala ataskani QR code ya mfuko wa mbolea iliyouzwa na taarifa za mbolea hiyo (aina, kampuni na uzito) zitaingia kwenye mfumo wa ruzuku;

* Kampuni itawasilisha hati ya madai kwa TFRA kwa mbolea yake ambayo imeuzwa;

* TFRA itaidhinisha malipo ya fedha ya ruzuku kwa kampuni husika; na Benki itafanya malipo ya ruzuku kwa kampuni.

Nafurahi kueleza wazi kwamba utekelezaji wa mpango huu wa ruzuku umewahusisha wadau mbalimbali wakiwemo Wizara ya Kilimo, TFRA, Kamati Tendaji ya Ruzuku, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Waingizaji/Wazalishaji wa Mbolea, Mawakala wa Mbolea, Taasisi za Fedha, Wakulima na wadau wengine.

Kila jambo tunalokusudia kama taifa linawezekana iwapo sote kwa pamoja tutakuwa makini kwa kuyapenda maendeleo ya nchi yetu.

BODI YA UHARIRI

DKT. STEPHAN NGAILO
- MWENYEKITI

MATILDA KASANGA
- KATIBU

DANIEL MAARIFA
- MJUMBE

RAYMOND KONGA
- MJUMBE

AZIZI MTAMBO
- MJUMBE

SALEHE KEJO
- MJUMBE

THERESIA SIRIWA
- MJUMBE

NURU MWASAMPETA
- MJUMBE

ALPHA NUHU
- MJUMBE

TAHARIRI

Ruzuku ya mbolea ni ukombozi kwa wakulima

WAKATI wa kilele cha sherehe za Nanenane zilizofanyika kitaifa jijini Mbeya mwaka 2022 Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alizindua rasmi mpango wa serikali wa utoaji ruzuku ya mbolea kwa wakulima.

Huu ni mpango kabambe wa kitaifa uliobuniwa kwa makusudi na serikali ili kukuza sekta ya kilimo nchini kwa kuwainua wakulima waongeze tija ya mazao mbalimbali siyo tu kwa faida yao, bali pia kwa faida ya uchumi wa taifa lao.

Kwa Tanzania, miongo mingi ijayo, kilimo kitaendelea kuwa ni uti wa mgongo wa taifa. Ndiyo maana serikali za awamu zote tangu uhuru zimekuwa zikitilia mkazo sekta hii.

Utekelezaji wa mpango wa ruzuku ya mbolea umehusisha wadau wengi kuanzia Wizara ya Kilimo, Mamlaka ya Udhhibiti wa Mbolea Tanzania, Kamati Tendaji ya Ruzuku, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Waingizaji/Wazalishaji wa Mbolea, Mawakala wa Mbolea, Taasisi za Fedha na Wakulima.

Wadau hawa wamehusishwa ili kuhakikisha kwamba mpango huu haukwami mahali popote. Nia ni kuhakikisha mbolea inamfikia mkulima kwa njia rahisi na kwa bei iliyopangwa na serikali badala ya kupitia njia zisizo halali kama vile ulanguzi wa bidhaa hiyo.

Ni jambo la kutia moyo kwamba Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, amekuwa mkali zaidi akiwakemea watu watakojaribu kuvuruga mpango huu kwa manufaa yao. Kwa hakika, huu ni mpango madhubuti wa kumkomboa mkulima katika harakati za kupambana na umaskini.

Kwa miaka mingi wakulima wa Tanzania wamekuwa wakiishi maisha duni na kukiona kilimo kama ni adhabu kwa sababu hawafaidiki na juhudi za kuwekeza katika sekta hiyo.

Kwa hakika yaliyopita si ndwele, sasa wakulima ni lazima waishikilie fursa hii ya mbolea ya ruzuku ili waweze kuinua hali zao za maisha katika nchi ambayo inathamini mchango wa kila mtu katika kukuza uchumi wa taifa.

Kama alivyosema Waziri Bashe wakati wa uzinduzi wa mpango huu wa ruzuku ya mbolea kwa wakulima wilayani Chamwino mkoani Dodoma, wakulima hawana budi kutumia nafasi hii kujisajili kwenye ofisi za Serikali za Vijiji vyao ili waweze kunufaika na mpango wa Serikali wa kuwapunguzia makali ya bei ya mbolea kupitia ruzuku.

Umuhimu wa mbolea katika maendeleo ya nchi, ni suala ambalo halina mjadala. Mikakati ya kuongeza matumizi ya mbolea nchini inaenda sambamba na kufikia uchumi wa kati wa viwanda kwa kuwa mbolea inayotumika katika kilimo ni msingi mkubwa wa uanzishwaji na maendeleo ya Sekta ya Viwanda.

Sekta ya Kilimo inatoa mazao mbalimbali ambayo ni malighafi inayotumika viwandani. Malighafi hiyo hutengeneza bidhaa mbalimbali baada ya kuyaongezea thamani mazao hayo kwa kuyasindika.

Kilimo kinatumia bidhaa zinazozalishwa na viwanda ikiwa ni pamoja na teknolojia, mbolea, viuatilifu na zana mbalimbali ambazo huchangia kuongeza tija.

Kuongezeka kwa matumizi ya mbolea nchini kutachochea kuanzishwa kwa viwanda vya kuchakata mazao yatokanayo na kilimo na hivyo kuongeza ajira nchini.

Kwa mantiki hiyo, matumizi sahihi ya mbolea katika sekta ya kilimo yataleta matokeo chanya katika sekta ya viwanda kwa kutoa malighafi kwa wingi kwa viwanda husika.

Isitoshe, uwepo wa viwanda vya mbolea nchini utahamasisha upatika-naji wa mbolea kwa wakati na kwa bei ya chini na hivyo kuongeza uzalishaji, tija na usalama wa chakula nchini, kudhibiti mfumuko wa bei za vyakula na kuinua kipato cha mkulima.

YALIYOMO



Matamano ya Rais Samia yafikiwa ujenzi kiwanda cha mbolea ITRACOM **Uk > 7**



Bashe awaonya watakaokiuka usajili ruzuku mbolea **Uk > 9**



Wakaguzi mbolea watakiwa kusimamia ubora **Uk > 10**



Bodi TFRA yakamilisha kazi kwa kishindo **Uk > 11**

Mbolea: Teknolojia yatumika kuziba udanganyifu **Uk > 12**

Maadhimisho Siku ya Mbolea Duniani 2022: Wakulima wajengewa uwezo... **Uk > 13**

Tanzania yashuhudia kasi ujenzi viwanda vya mbolea **Uk > 18**

Utaratibu wa kupata Usajili na Leseni za Biashara ya mbolea **Uk > 28**

Rais Samia: Simamieni vema Mpango wa ruzuku ya mbolea



Rais Samia Suluhu Hassan akikata utepe ikiwa ni ishara ya kuzindua rasmi mpango wa ruzuku za mbolea zitakazoanza kutolewa kwa wakulima kuanzia tarehe 15 Agosti, 2022 wakati wa maadhimisho ya sikukuu ya wakulima nanenane yaliyofanyika katika viwanja vya Mwakangale Jijini Mbeya.

Na NURU MWASAMPETA

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan amewataka wataandaji wote katika mnyororo wa thamani wa kilimo kusimamia kwa umakini mkubwa mpango wa serikali wa utoaji wa mbolea za ruzuku katika msimu wa kilimo wa 2022/2023.

Akizindua rasmi Mpango huo wakati wa kilele cha Sikukuu ya maonesho ya wakulima, Nanenane Rais Samia alimuagiza Waziri wa Kilimo Hussein Bashe kuanza utekelezaji ifikapo tarehe 15 Agosti, 2022 ili kutoa nafasi kwa wakulima kujiandaa kuanza msimu wa kilimo kwa mwaka 2022/2023.

Pamoja na uzinduzi huo, Rais Samia alikiri kuona ari ya watumishi wa Wizara ya kilimo na taasisi zake kuanza kutekeleza kwa dhati mpango wa utoaji wa mbolea ya ruzuku na mipango mingine inayotekelezwa na kusimamiwa na wizara hiyo.

Akizungumza kuhusu maamuzi ya serikali kutoa ruzuku, Rais Samia aliwataka wakulima kutumia fursa hiyo kuzalisha kibiashara ili kupata chakula cha kutosha pamoja na cha kuuza nje ya nchi na hivyo kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla na aliongeza kuwa, Serikali haitajikita kwenye kutoa ruzuku za mbolea kwa miaka yote.

Aliongeza kuwa, uzalishaji huo utafanya Serikali kuanzisha mfuko wa pembejeo utakotumika wakati kunapotokea dharura na kusa-

babisha kupanda kwa bei za pembejeo za kilimo, hivyo mfuko huo kutumika kuwapunguzia wakulima hadha ya bei za pembejeo.

Pamoja na mpango wa Serikali wa kutoa ruzuku za mbolea, Rais Samia alieleza mipango mahususi ya kuongeza uzalishaji wa mbolea ndani ya nchi na kueleza uwepo wa kiwanda cha Itracom Fertilizer Limited kinachojengwa mkoani Dodoma na kile cha Minjingu Wilaya ya Babati Mkoani Manyara kuwa vitapunguza adha ya upatikanaji na bei ya mbolea kwa wakulima.

Aliongeza kuwa, katika kuvijengea uwezo viwanda vya mbolea vya ndani, Serikali inamjengea uwezo mwekezaji wa kiwanda cha Minjingu ili awe na uwezo wa kupata mikopo itakayomsaidia kuendeleza kiwanda na hivyo kuongeza uzalishaji,

Pamoja na hayo, Rais amezitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha wanasimamia zoezi la utoaji wa ruzuku ya mbolea na kuwataka kutoacha jukumu hilo kusimamiwa na Wizara ya Kilimo pekee.

Aidha, Rais Samia alizitaka Wizara ya kilimo pamoja na Wizara ya Fedha kuhakikisha zinatoa fedha za ruzuku kwa wakati ili wakulima wapate mbolea kwa wakati na hivyo kuzalisha kwa wingi na kwa tija.

Mwisho Rais alitoa wito kwa wakulima wote kujisajili na kubainisha kuwa mbeleni vitambulisho vitatolewa kwa wakulima ili kuwawezesha kupata huduma mbalimbali zinazohusiana na

masuala ya kilimo.

Kwa Upande wake Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe alimshukuru Rais kwa kuridhia kushuka kwa bei za mbolea kwani kilikuwa kilio kikubwa kwa wakulima kwa msimu uliopita.

Akiwasilisha bei za mbolea kwa Rais Samia kabla ya uzinduzi, Waziri Bashe alisema mbolea aina ya DAP wastani wa bei kabla ya ruzuku ni 131,676 baada ya ruzuku itauzwa shilingi 70,000 na serikali itachangia kwa shilingi 61,676, mbolea ya UREA kabla ya ruzuku inauzwa kwa wastani wa 124,734 baada ya ruzuku mkulima atanunua kwa shilingi 70,000 ambapo serikali itachangia kiasi cha shilingi 54,734.

Mbolea nyingine zitakazotolewa katika ruzuku ni CAN kabla ya ruzuku ni shilingi 108,156 baada ya ruzuku itauzwa shilingi 60,000, mbolea aina ya SA inauzwa shilingi 82,852 baada ya ruzuku itauzwa shilingi 50,000 na NPK's zinauzwa kwa wastani wa shilingi 122,695 baada ya ruzuku zitauzwa 70,000 na kiasi kinachozidi serikali itachangia hivyo kupunguza mzigo wa bei ya mbolea kwa mkulima.

Kwa upande wake Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, alipongeza Serikali kwa kusimamia na kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi yenye lengo la kuleta mapinduzi kwenye sekta ya kilimo.

"Ilani ya uchaguzi 2020/2025 imebeba ajenda ya kilimo kama kipaumbele kikuu kuikuza sekta hii kukuza mchango wake ifikapo 2030" Chongolo aliongeza.



Matumizi ya mbolea katika mazao ya mizizi

Na Aziz Mtambo



MAANA YA MAZAO YA MIZIZI

Mazao ya mizizi ni mazao ambayo sehemu yake ya chini (Mizizi) ndio hutumika kama chakula kuuzwa baada ya kukomaa, mazao haya yanaweza kuwa ya aina ya mbogamboa kama vile karoti, vitunguu, turnips na jamii nyingine za aina hii au mimea mikubwa kama vile mihogo, viazi na jamii yake na mazao haya yanafanana katika baadhi ya kanuni za kilimo.

Baada ya kujua maana ya mazao ya mizizi leo tutaangalia kwa uchache matumizi ya mbolea katika mazao haya kwa kuangalia zaidi zao la Muhogo

Imezoeleka kuwa, mazao ya mizizi hasa aina ya mihogo ni mazao ambayo hayahitaji mbolea katika kilimo chake kwani ni mazao yanayostahili ukame pia ni mazao ambayo yanalimwa katika maeneo ya hali ya hewa mbalimbali. Lakini pamoja na hilo tunatambua kuwa ili mmea uweze kukua na kutoa mazao kwa wingi basi ni lazima udogo/ardhi inayotumika iwe na virutubishi vya kutosha ili mmea uweze kupata mahitaji yake. Katika zao la Muhogo mbolea huweza kuongeza uzalishaji kutoka tani 10 hadi 16 kwa hekta endapo mbolea itatumika kwa ufasaha na kuzingatia kanuni za kilimo bora.

Ili kupata mazao mengi na tija katika kilimo cha mihogo ni lazima kuzingatia kwanza kanuni za kilimo bora kama ilivyo katika mazao mengine kama vile:

- i. Kuchagua shamba
- ii. Kupima afya ya udogo
- iii. Kuandaa shamba kwa wakati
- iv. Kutumia mbegu/miche bora
- v. Kupanda kwa wakati
- vi. Kuweka mbolea kwa wakati
- vii. Kupalilia kwa wakati
- viii. Kuzuia wadudu na magonjwa kwa wakati
- ix. Kuvuna kwa wakati
- x. Kuhifadhi kwa kufuata njia bora za kuhifadhi

NB: hakikisha unafuata ushauri toka kwa afisa kilimo wa eneo husika.

Matumizi ya mbolea katika zao hili la muhogo kwani ni moja katika ya kanuni bora za kilimo. Baada ya kupima udogo na kujiridhisha ni kwa kiasi gani ardhi/shamba linaupungufu au lina rutuba kiasi gani basi unaweza kutumia mbolea ili kuongeza kiasi cha rutuba au virutubisho vilivyopungua katika ardhi ardhi/udongo

Matumizi ya mbolea

Zao la mihogo ni kati ya mazo ya muda mrefu na linahitaji kiasi cha kutosha cha virutubisho pidi linaopokuwa shambani virutubisho hivyo ni kama vile Nitrojeni, Fosiforasi, Potashiamu Maginiziam na virutubishi vingine vidogovidogo kama Boron, Zinc Calcium n.k katika kipindi cha mzunguko wa maisha yake.

Muhogo ni zao linalotumia kiasi kikubwa cha virutubishi na kuweza kupelekea kupunguza virutubishi ardhini/udongo, Mbolea hutakiwa kuweka ili kuweza kurudisha kiasi cha virutubisho vilivyopungua katika udongo na kuweza kuendelea kutoa mazao mengi kwa kiwango kinachotakiwa, kwa kuzingatia hili basi mkulima anashauliwa kutumia mbolea za NPK kama vile N:P:K 17:17:17 au 15:15:15 lakini pia unaweza kutumia mbolea zenye virutubishi kimoja kimoja kama vile DAP, UREA, SSP, MOP pindi mbolea

hizo zinapokosekana (*gardening tips*).

Matumizi ya mbolea huweza kuongeza uzalishaji/tija katika zao hili endapo mbolea itatumika kwa kiasi kiachotakiwa au kushauriwa.

Uwekaji wa mbolea katika mihogo

Kabla ya kuweka mbolea za viwandani kipindi cha kuandaa shamba na ukiwa umeshajua shamba linaupungufu wa virutubisho gani basi unaweza kuanza kwa kuweka chokaa kilimo (ili kusawazisha kiasi cha pH katika udongo), gypsum, mbolea za kienyeji (mbolea vunde) au masalia ya mazo ya awali yaliyoza ili kuongeza baadhi ya virutubishi vilivyopotea lakini pia kuweka hali ya msawazo ya udogo, na hakikisha unachanganya na udongo vzuri.=

Kiasi cha mbolea kwa hekta ni kama ilivyooneshwa katika jedwali hapo chini kwa mbolea za NPK lakini kiasi hcho ni lazima ukigawe mara tatu kulingana na vipindi vya uwekaji.

Jedwali: kiasi cha mbolea ya NPK 15:15:15 na NPK 17:17:17 kinachohitajika.

Mbolea	Kg kwa hekta	Gm kwa mmea
NPK 15:15:15	800 (16 bags)	80
NPK 17:17:17	700 (14 bags)	70

Source: AFRICA soil health consortium

Vipindi vya uwekaji wa mbolea:

A. Kipindi cha kwanza cha uwekaji mbolea:

- Wiki ya 6 Baada ya kupanda,

Wiki ya sita unashauliwa kuanza kuweka mbolea ili kuweza kurudisha au kuongeza kiasi cha virutubisho ambavyo vimepungua katika udongo na kuwezesha mmea kukua na kutoa mazao kwa tija, unaweza kutumiambolea kama vile za NPK 15:15:15 au NPK 17:17:17 zitakazoweza kuongeza uzalishaji hadi kufikia tani 16 kwa hekta

Kiasi hiki cha mbolea hugawanywa mara tatu katika kipindi cha msimu mmoja yaani $800/3 = 266.6$ kg kwa hekta na kuwekwa 3 (Source: AFRICA soil health consortium)

B. Kipindi cha pili cha uwekaji mbolea:

- Wiki ya 10 hadi 12.

Kipindi cha pili kiasi cha mbolea kilichoweza mwanzo kitatakiwa kuwekwa tena wiki 10 hadi 12 baada ya kupanda.

C. Kipindi cha tatu cha uwekaji mbolea

- Wiki ya 16 hadi ya 20.

Awamu ya tatu ambayo ni ya mwisho kwa msimu, kiasi kilichobaki kama ilivyotumika mwanzo basi kitawekwa wiki ya 16 hadi ya 20 baada ya kupanda lakini itategemea na vipindi vya mvua na usiweke kipindi ambacho mvua zimeisha.

Katika kuongeza uzalishaji basi mkulima anashauliwa kufuata jedwali lililopo chini linaloonesha matumizi ya mbolea kulingana na uzalishaji.

>>> **Inaendelea Uk. 6**

Jedwali: Linaonesha kuwa ikiwa mkulima anahitaji kuongeza uzalishaji toka tani 10 hadi 16 kwa hekta

Makadirio ya mavuno	NPK 15:15:15		NPK 17:17:17	
	Jumla ya kg kwa hekta (50kg bag)	Jumla ya gm kwa mmea	Jumla ya kg kwa hekta (50kg bag)	Jumla ya gm kwa mmea
10	0	0	0	0
11	133(2.7)	13	117 (2.3)	12
12	266 (5.3)	27	234 (4.7)	23
13	400(8)	40	350 (7)	35
14	533 (10.7)	53	468 (9.4)	47
15	666 (13.3)	67	585 (11.7)	59
16	666 (16)	80	700 (14)	70

Source:AFRICA soil health consortium

Jinsi ya kuweka mbolea katika mmea.

- i. Mbolea huwekwa sentimeta 20 kutoa katika shina, chimba mfereji wenye Kina cha sentimeta 5 katika shape ya nusu duara, funika mfereji kwa udon-

- go. Kumbuka hii hufanyika kila msimu, hakikisha unatumia kijembe kidogo ili kulinda kutochubua mizizi
- ii. Weka kiasi kinachotakiwa katika mfereji
- iii. Funika vizuri mfereji kwa udongo

Mbolea za virutubisho kimojakimoja pia zinaweza kutumika katika kilimo cha mihogo na kulieta ufanisi zaidi kwani zinatumiwa kwa kulenga moja kwa moja kirutubishi kilichokosekana katika shamba tofauti na mbolea za NPK kwani unaweza kuweka virutubishi ambavyo haviitajiki kwa wakati huo.

Aina za mbolea hizo ni kama vile;

- i. Urea hutoa Naitrojeni (N)
- ii. TSP hutoa Fosiforasi (P)
- iii. Potashiamu Chrolide inatoa Potashiam (K)
- iv. DAP inatoa Fosiforasi (P)

Na mbolea nyingine zinazotea virutubisho hivyo.



Jinsi ya kuweka mbolea katika zao la muhogo nusu duara (10-20 sm)

Jedwali: Linaonesha matumizi ya mbolea za kirutubisho kimojakimoja

	Mbolea zenye fosiforas (P)		Mbolea zenye Naitrojeni (N)		Jumla ya kg kwa hekta (50kg bag)	Jumla hya gm kwa mmea
	Jumla ya kg kwa hekta (50kg bag)	Jumla ya gm kwa mmea	Jumla ya kg kwa hekta (50kg bag)	Jumla ya gm kwa mmea		
Mfano 1: TSP, Urea, MOP	TSP 54 (1 bag)	TSP 5	Urea 260 (5.2 bags)	Urea 26	MOP 173 (3.5 bags)	Mop 17
Mfano 2: DAP, Urea MOP	DAP 54 (1bag)	DAP 5	Urea 240 (4.8 bags)	Urea 24	MOP 173 (3.5 bags)	MOP 17

Utakapotumia mbolea hizi basi unaweza kupata kiasi kinachohitajika kwa mmea.

Faida za kutumia mbolea za kirutubisho kimojakimoja;

Uwekaji wa mbolea za virutubisho kimoja ni tofauti na uwekaji wa NPK kwakuwa huruhusu kuweka virutubisho hivyo pindi tu vinapohitajika N, P, K.

TSP huwekwa katika kipindi cha kupanda, kwa kuwa inatoa P na Urea na KCL huwekwa katika vipindi vitatu (3) wiki ya 4-6, wiki ya 10-12 na wiki ya 16-20 baada ya kupanda kama ilivyo katika uwekeji wa N:P:K

Pamoja na matumzi ya mbolea za viwandani tunashauriwa kutumia mbolea za asili kama vile mbolea vunde (Compsite Manure), mabaki ya mazao yaliyoza/kuachwa shambani baada ya kuvuna lakini pia matumizi ya samadi ili kupunguza gharama ya kununua mbolea za viwandani kwani ni gharama ukilinganisha na mbolea za asili katika kilimo cha mihogo lakini itahitajika kwa wingi sana katika shamba ili kufikia kiasi cha virutubisho vinavyotakiwa shambani.



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kasim Majaliwa Majaliwa akiwasili katika kiwanda cha mbolea cha Itracom Jijini Dodoma na kupokelewa na Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe (mwenye kofya kulia) na viongozi wengine wa serikali alipofika kujijonea maendeleo ya ujenzi wa kiwanda hicho tarehe 20 Desemba, 2022.

Matamano ya Rais Samia yafikiwa ujenzi kiwanda cha mbolea ITRACOM



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kasim Majaliwa Majaliwa (wa pili kutoka kulia) akiambatana na viongozi walioshiriki kwenye ziara yake ili kukagua utendaji kazi wa kiwanda cha Itracom kilichopo Nala jijini Dodoma tarehe 20 Desemba, 2022.

Na NURU MWASAMPETA

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kassim Majaliwa Majaliwa amesema matamano ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha mbolea ya kutosha inazalishwa nchini badala ya kutegemea kuagiza nje yametimia baada ya kiwanda cha mbolea cha Itracom kilichopo Nala jijini Dodoma kuanza uzalishaji.

Waziri Mkuu Majaliwa aliyasema hayo tarehe 20 Desemba, 2022 alipotembelea kiwanda hicho ili kujionea hatua iliyofikia na kukagua shughuli zinazoendelea kiwandani hapo.

Alisema uwekezaji huo ambao unaenda sambamba na ujenzi wa viwanda vingine vitatu, kiwanda cha chokaa ya kilimo, vifungashio vya mbolea na kiwanda cha maziwa utaisadia Serikali katika kukabiliana na changamoto ya ajira.

“Kuna fursa nyingi katika kiwanda hiki ikiwemo upatikanaji wa mbolea ya uhakika na kwa gharama nafuu.” Alisema Majaliwa.

Majaliwa amekiri kuwa ahadi ya mwekezaji ya kuanza uzalishaji mwezi wa 8/9, 2022 imetimia kwani tayari uzalishaji umeanza na wakulima watanunua mbolea hizo kwa bei ya ruzuku.

Waziri Mkuu Majaliwa alisema eneo hilo la uwekezaji lazima liwe na huduma zote muhimu zinazohitajika ili kukiwezesha kiwanda hicho kuendelea na uzalishaji. Huduma hizo ni pamoja na ujenzi wa miundombinu ya uhakika ya

>>> **Inaendelea Uk. 8**



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kasim Majaliwa Majaliwa (aliyeweka mkono kwenye mfuko wa mbolea) akisoma maelezo yaliyo juu ya mfuko huko alipotembelea kiwanda hicho hivi karibuni.

<<< **Inatoka Uk. 7**

barabara, maji, mawasiliano pamoja na nishati ya umeme.

Vilevile, Waziri Mkuu Majaliwa alitumia fursa hiyo kutoa rai kwa Watanzania wanaofanya kazi kiwandani hapo wafanye kazi kwa bidii, weledi na uaminifu wa hali ya juu ili wawe mabalozi wazuri kwa wawekezaji wengine watako kuja kuwekeza nchini. "Mkifanyakazi kwa bidii na uaminifu mtawarahisishia na wengine kupata kazi." Aliongeza Waziri Mkuu

Akizungumzia utofauti wa mbolea inayozalishwa na kiwanda hicho, Majaliwa alisema mbolea hiyo inazalishwa kulingana na mahitaji yaliyobainishwa baada ya upimaji wa udongo na kubaini virutubisho vilivyopungua kwa kila mkoa nchini kutokana na teknolojia ya uzalishaji mbolea ulivyo.

Naye Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe alisema, katika kuhakikisha viwanda vya mbolea ndani ya nchi vinafikia malengo, Serikali imefuta kodi zote na hivyo kuvifanya viwanda vya ndani vizalishe kwa hali ya juu.

Alieleza kuwepo kwa changamoto kwenye usambazaji wa mbolea za ruzuku kwa msimu huu wa kilimo kutokana na kuwa mfumo unao-tumika ni mpya na kukiri kuwa kadri tunavyoen-delea changamoto zote za utoaji na usambazaji wa mbolea za ruzuku zitatatuliwa.

"Tutajaribu kwa kadri ya uwezo wetu ku-



Viongozi wa serikali na kiwanda wakifuatilia mkutano na Waziri Mkuu Kasim Majaliwa mara baada ya kutembelea maeneo mbalimbali ya kiwanda cha mbolea Itracom Jijini Dodoma na kupewa maelezo katika ziara iliyofanyika Desemba 20, 2022.

fikisha mbolea kwenye vitongoji na vijiji ili kuwawezesha wakulima kulima kwa tija," alihitimisha Bashe.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa kiwanda cha Itracom Nduimana Nazir alimpongeza Rais Samia kwa kuvutia uwekezaji nchini na kukiri kuwa wanaendesha shughuli zao kwa am-

ani na utulivu.

Ameshukuru kwa ushirikiano wanaoupata kutoka Wizara ya Kilimo na taasisi zake ikiwemo Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Bashe awaonya watakaokiuka usajili ruzuku mbolea



Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, (Kushoto) na Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, David Silinde, wakiwa wamenyanhya mfuko wa mbolea ya ruzuku wa kilo 50 wakati wa hafla ya uzinduzi wa usajili wa wakulima utakaowawezesha kunufaika na mbolea ya ruzuku itakayoanza kutolewa msimu wa kilimo kwa mwaka 2022/2023.

Na NURU MWASAMPETA

Mamlaka ya Udhhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) imetakiwa kuwasilisha majina ya kampuni zitakazokiuka utaratibu wa kusajiliwa ili zilishiriki zoezi la usambazaji wa mbolea za ruzuku kwa wakulima nchini.

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, ameon-

ya kwamba yuko tayari kufuta leseni za usajili wa kampuni zote zitakazokiuka utaratibu wa kusajiliwa.

Alitoa onyo hilo Julai 4 mwaka huu wakati wa Uzinduzi wa Mfumo wa Kidijitali wa Usajili wa Wakulima na Mwongozo wa Utoaji wa Mbolea ya Ruzuku kwa msimu wa kilimo 2022/2023 uliofanyika wilayani Chamwino,

Dodoma.

Alisema makampuni yote yatakayohusika na uingizaji mbolea za ruzuku lazima yafuate taratibu za serikali ili kuepuka udanganyifu.

"Sitakuwa tayari kuziangalia kampuni zitakazofanya udanganyifu, nahitaji kuona kila kampuni inafuata utaratibu uliowekwa na Serikali wa uingizaji wa mbolea nchini," alisema Bashe.

Pamoja na hayo, waziri huyo alionya kwamba mfanyabiashara yeyote anayejandaa kuingia kwenye mfumo wa mbolea ya ruzuku akidhani itakuwa kama ilivyokuwa wakati wa vocha atakuwa amepoteza muda wake.

"Yeyote anayejandaa kuingia kwenye mfumo wa ruzuku za vocha itakuwa imekula kwake," Hakufafanua.

Akizungumzia kuhusu vipaumbele vya utoaji ruzuku ya mbolea, Bashe alisema serikali itatoa kipaumbele kwa viwanda vya ndani ili kuchochea uwekezaji katika tasnia hiyo nchini.

Katika hatua nyingine, Bashe aliomba TAMISEMI kuondoa adhabu ya kulima kwa wanafunzi waliofanya makosa kwa kufanya hivyo kunawageza watoto wachukie kilimo wakiwa wadogo.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Andrew Masawe, alisema utoaji wa mbolea ya ruzuku ni moja kati ya mikakati ya kufanikisha agenda 10/30 inayohitaji kuona mchango wa sekta ya kilimo unakuwa kwa asilimia 10 ifikapo 2030.

Naye Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, aliwaagiza Wakuu wa Mikoa na Wilaya kufuatilia kwa kina Maofisa Kilimo kuanzia ngazi ya taifa hadi kijiji na kuhakikisha wana-tekeleza majukumu yao ya kitalaamu badala ya kinyume cha utaalum wao.

Alibainisha kuwa serikali inafanya hivyo kwa sababu inajua maafisa kilimo wengi wanafanya kazi tofauti na taaluma yao iliyowaweka kazini.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhhibiti wa Mbolea Tanzania, Dkt. Stephan Ngailo, aliishukuru Wizara ya Kilimo kwa ushirikiano na maelekezo inayoyatoa katika kuhakikisha mkakati wa usambaji mbolea ya ruzuku unafanikiwa.

Alisema katika kuhakikisha suala la utoaji ruzuku linafanikiwa TFRA ikishirikiana na CRDB Bank na Kampuni ya Mawasiliano ya Vodacom wameandaa mfumo wa kidigitali wa usajili, mwongozo pamoja na fomu kwa ajili ya usajili wa wakulima.

Alisema TFRA iko tayari kutekeleza maa-gizo iliyopewa na wizara na kuhakikisha wakulima ndiyo wanaonufaika na mbolea hizo.

Wakaguzi mbolea watakiwa kusimamia ubora



Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhhibiti wa Mbolea Tanzania Dkt. Stephan Ngailo akizungumza wakati wa kufunga mafunzo ya wakaguzi wa mbolea yaliyofanyika mkoani Morogoro Novemba 17, 2022 katika ukumbi wa taasisi ya Misisu.

Na **MATILDA KASANGA**

Wakaguzi wapya 30 wanaosimamia tasnia ya mbolea wametakiwa kuwaweze-sha wakulima kupata bidhaa yenye ubora.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Dkt. Stephan Ngailo, amesema kutokana na ukubwa wa nchi, taasisi yake itaendelea ku-

Baada ya kupewa mafunzo hayo Halmashauri yake itahakikisha kuwa utendaji wake utazingatia sheria, kanuni na miongozo iliyowekwa na Mamlaka ili kuleta ufanisi unaotarajiwa...

toa mafunzo kwa wakaguzi ili kuhakikisha kuwa kila halmashauri nchini inakuwa mkaguzi wa mbolea.

Dkt. Ngailo aliwataka wakaguzi kutatua changamoto za upatikanaji wa takwimu za mahitaji na matumizi ya mbolea katika ngazi za halmashauri pamoja na kutekeleza majukumu yao kwa uadilifu, ikiwemo kutokupokea zawadi kutoka kwa wafanyabiashara wa mbolea kwa sababu watashindwa kusimamia ipasavyo sheria, kanuni na miongozo iliyowekwa kusimamia tasnia hiyo.

Alitoa wito huo kwa wakaguzi hao mwishoni mwa mafunzo yao ambapo aliwataka kutenda haki bila upendeleo.

Afisa Kilimo wa Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi, Sagile Samweli, alisema wakaguzi wa mbolea wamejengewa uwezo wa kusimamia maamuzi ya kitaalam yanayohusu ubora wa mbolea.

Alisema kuwa baada ya kupewa mafunzo hayo Halmashauri yake itahakikisha kuwa utendaji wake utazingatia sheria, kanuni na miongozo iliyowekwa na Mamlaka ili kuleta ufanisi unaotarajiwa.

Pia washiriki hao waliomba TFRA iwekeke mazingira wezeshi ili waweze kutekeleza majukumu hayo mapya ya ukaguzi wa mbolea ikiwemo kuwapatia vitendea, kazi ombi ambalo lilikubaliwa.

Mkurugenzi wa Huduma za Udhhibiti wa TFRA, Happiness Mbelle, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuhakikisha kuwa wakulima kote nchini wanapata mbolea bora ili kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao mbalimbali.

TFRA kila mwaka huandaa mafunzo ya wakaguzi wa mbolea ili kuongeza idadi ya wadhhibi wa mbolea watakaoweza kufika katika maeneo yote nchini.



Watumishi pamoja na Wahitimu wa mafunzo ya ukaguzi wa mbolea yaliyofanyika mkoani Morogoro Novemba 14 hadi 17, 2022 wakiwa katika picha ya pamoja na wawezeshaji kutoka TFRA.



Wajume wa iliyokuwa Bodi ya Wakurugenzi wa TFRA wakiwa katika picha ya pamoja

Bodi TFRA yakamilisha kazi kwa kishindo

Na TERESIA SIRIWA

Bodi ya Wakurugenzi wa Mamlaka ya Mbolea Tanzania (TFRA) imekamilisha shughuli zake kwa kishindo Agosti mwaka 2022 tangu ilipoteuliwa Septemba 2019.

Ikiwa na wajumbe 12, Bodi hiyo ilitekeleza majukumu yake kwa ufasaha kama yalivyoainishwa katika Kifungu cha 5 (1) cha Sheria ambayo ni kusimamia masuala yote iliyokabidhiwa kwa miezi 31 ambapo imefanya vikao 11 vya kiutendaji.

Sekretarieti inayoandaa na kusimamia vikao vya Bodi hiyo imeeleza kuwa chombo hicho kimatekeleza majukumu yake kwa ufanisi kupitia vikao na kutoa maelekezo kwa Menejimenti.

Pia Bodi hiyo imekuwa ikifuatilia utendaji wa menejimenti kwa kupitia nyaraka mbalimbali za utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka na kutatua changamoto mbalimbali zilizojitokeza kwa maslahi ya Taasisi na Taifa kwa ujumla.

Katika kipindi cha miaka mitatu ya usimamizi wa Menejimenti ya TFRA, Bodi imewezesha kufanikisha upatikanaji wa Muundo wa Utumishi, Maendeleo ya Utumishi, sambamba na kuongezeka kwa watumish kwa asilimia 88.75, ikijumuisha watendaji wa ofisi za kanda (Mbeya, Mwanza, Tabora na Arusha).

Ongezeko la watumishi limewezesha kuanzishwa kwa chama cha wafanyakazi wa Serikali Kuu na Afya (TUGHE, tawi la TFRA), pamoja na Baraza la Wafanyakazi.

Bodi imefanikisha utekelezaji wa ukarabati wa majengo ya taasisi na kuongeza ufanisi wa watumishi kufanya kazi zao katika jengo la Killimo. Pia Bodi imefanikisha kuanza kwa utekelezaji wa ujenzi wa maabara kwa kutumia fedha za ndani kupitia utaratibu wa Force Account.

Kukamilika kwa Maabara kutasaidia kufanya uchambuzi wa mbolea kwa wakati na kwa ubora unaokubalika.

Hali kadhalika, Bodi imefanikisha kuanzishwa na kutumika kwa mfumo wa kielektroniki wa mbolea (FIS-Fertilizer Information System) ambao umeongeza ufanisi katika utoaj huduma mbalimbali za Mamlaka, ikiwemo huduma za usajil wa mbolea, usajil iwa wafanyabiashara wa mbolea na utoaji wa vibali vya uingizaji na usafirishaji wa mbolea.

Kupitia mfumo huo na ongezeko la watumishi, utoaji huduma katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo ofisi za Kanda; Kanda ya Ziwa, Kanda ya Kati, Kanda ya Kaskazini na Kanda ya Nyanda za Juu Kusin umeimarika.

Kwa kukupitia Bodi, sekretarieti imeeleza, kwamba TFRA imetambulika zaidi kitaifa na kimataifa, kwa kujitangaza kupitia vyombo

mbalimbali vya habari, redio, televiseheni na magazeti. kwa kushirikiana na taasisi za umma na wadau mbalimbali. Kwa kupitia biashara ya mbolea, Mamlaka imejitangaza kimataifa katika nchi mbalimbali kama Saudi Arabia, Morocco, Urusi na China. Pia imeweza kushirikiana na wawekezaji wa viwanda vyambolea nchini kama Burundi (FOMI).

Katika kipindi cha miaka mitatu Mamlaka imefanikiwa kuongeza viwanda vya mbolea na visaidizi nchini kutoka 12 hadi 16 kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara na Kituo cha Uwekezaji TIC). Katika uhamasishaji wauzalishaji wa mbolea nchini, Bodi imefanikisha kuongezeka kwa upatikanaji wa mbolea nchini kwa asilimia 41, matumizi ya molea kwa ongezeko la asilimia 31 na ongezeko la mbolea zilizosajiliwa kwa asilimia 45.

Mafanikio haya ni jitihada za Bodi za kutatua changamoto mbalimbali kwenye tasnia ya mbolea na kutengeneza mazingira wezeshi kwa wawekezaji. Hakika, Bodi ya tatu ya TFRA imemaliza muda wake kwa kuacha mafanikio makubw akwa TFRA na wadau wa tasnia ya mbolea kwa ujumla.

Pamoja na mafanikio hayo machache kati ya mengi ambayo hayajaainishwa, Bodi hadi ninamaliza muda wake Septemba 8, 2022 imeondoka na matarajio makubwa ikiwemo kuwepo kwa maabara ya mbolea, kuimarisha ofisi za kanda, kuongeza idadi ya wakaguzi wa mbolea nchini, kuongeza utii wa sheria kwa asilimia 90 kuongezeka kwa viwanda vya uzalishaji wa mbolea na kuwa na mfumo wa uhakika wa upatikanaji wa takwimu.



Kaimu Meneja wa Mamlaka ya Udhhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) Kanda ya Kaskazini, Gothard Liampawe (katikati) akimwelekeza mkulima, Hussein Rajab (mwenye kofia) kulipia na kuchukua risiti baada ya mauziano ya mbolea kukamilika. Mwenye T shirt nyeusi ni Athman Hassan Meneja wa kampuni la mbolea la ETG input Babati.

Mbolea: Teknolojia yatumika kuziba udanganyifu

Na SALEHE KEJO

Katika mwaka wa fedha wa 2022/2023 serikali imetenga shilingi bilioni 150 kugharamia ruzuku ya mbolea itakayotolewa kwa wakulima wote nchini.

Lengo la kutoa ruzuku hii ni kupunguza makali ya bei ya mbolea kwa wakulima ili kuongeza uzalishaji na tija katika kilimo, kuimarisha usalama wa chakula nchini na kuongeza mchango wa sekta ya kilimo katika pato la taifa.

Ili kuhakikisha kuwa ruzuku inatumika kwa malengo yaliyokusudiwa na kunufaisha wakulima wote, utoaji wa ruzuku unazingatia mahitaji halisi ya mkulima kulingana na taarifa za usajili. Katika kutekeleza Mpango wa utoaji wa mbolea za ruzuku serikali imeandaa mfumo wa kidigitali ambao unatumika kuwapa ruzuku ya mbolea wakulima wote nchini katika msimu wa kilimo wa 2022-2023.

Meneja wa TEHAMA na Takwimu Robert Mtendamema amesema Mamlaka imepewa jukumu la kusimamia mpango wa ruzuku ya mbolea ambao unafanyika kwa njia ya kidigitali ili kuondoa udanganyifu uliojitokeza kwenye ruzuku za mbolea za miaka ya nyuma.

Mtendamema anasema Mfumo wa kidigitali (Digital Fertilizer Subsidy Distribution and Payment) ambao umefadhiliwa na benki ya CRDB ndio unatumika kutekeleza mpango wa ruzuku ya mbolea kwa mwaka 2022. Mfumo huu unasajili wakulima, wafanyabiashara wakubwa

(waingizaji na wazalishaji) na wafanyabiashara wadogo (Mawakala) wa mbolea kote nchini.

“Mfumo wa ruzuku wa kidigitali mpaka tarehe 30/11/2022 umeshasajili wakulima 2,450,130, umesajili wafanyabiashara wadogo wa mbolea 2,902, waingizaji na wazalishaji wa mbolea 33,” anaeleza Mtendamema.

Mfumo wa ruzuku wa kidigitali unatuma meseji kwa wakulima mara tu wanaposajiliwa na wanaponunua mbolea ya ruzuku. Vile vile mfumo umesajili aina zote za mbolea zilizopo kwenye mpango wa ruzuku pamoja na bei zake kwa kila mahala nchi nzima.

Mtendamema anaendelea kusema mfumo wa kidigitali umewezesha wakulima kununua mbolea kwa kutumia namba maalumu walizopewa baada ya kusajiliwa kwenye mfumo.

Wafanyabiashara wanatumia mfumo kuu-

Mamlaka inapanga mgawanyo wa mbolea Pamoja na QR codes za mbolea kwa wafanyabiashara wakubwa ambao wanawapatia mawakala wadogo kwa ajili ya kufikisha mbolea hizo kwa mkulima.

za mbolea kwa kutumia App maalum ya mauzo (Agrodealer tool) ambayo inapokea namba ya mkulima na kusoma QR code ya mfuko wa mbolea ili kutambua mbolea imeuzwa kwa mkulima yupi na kwa kiasi gani cha fedha.

Kwa mujibu wa wataalamu wa TEHAMA mfumo wa ruzuku wa kidigitali unatumika kulipa wafanyabiashara stahiki wa mbolea wanaotakiwa kulipwa kwa kuzingatia taarifa za mgawanyo wa mbolea waliyopewa, mauzo ya mbolea hiyo kwa wakulima.

Mamlaka inapanga mgawanyo wa mbolea pamoja na QR codes za mbolea kwa wafanyabiashara wakubwa ambao wanawapatia mawakala wadogo kwa ajili ya kufikisha mbolea hizo kwa mkulima.

Mpaka kufikia Novemba 30, 2022, mfumo wa ruzuku umetoa huduma kwa wakulima 380,375 nchini kote wakiwa wamehudumiwa kiasi cha tani 113,767.78 za aina mbalimbali za mbolea aina mbalimbali. Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhhibiti wa Mbolea Tanzania Dkt. Stephan Ngailo, mfumo wa ruzuku umekuwa na mafanikio makubwa kwa kuwabaini wafanyabiashara wasio waaminifu wanaotumia namba za wakulima kuuza mbolea bila wakulima hao kuwa na taarifa za manunuzi hayo.

Mfumo wa ruzuku umebaini wafanyabiashara hao wasio waaminifu kupitia meseji za manunuzi za mbolea ya ruzuku zinazotolewa na mfumo huu.

Dkt. Ngailo anasema mfumo wa ruzuku ambao unaonyesha kiasi cha mbolea kilichopo nchini pamoja na mahala ilipo umesaidia kutambua maeneo yenye uhaba wa mbolea hivyo serikali kuhakikisha huduma ya mbolea inapelele kwa sehemu hizo haraka iwezekanavyo.

Matumizi ya teknolojia katika utekeleza wa mpango wa serikali wa utoaji wa mbolea za ruzuku katika msimu wa kilimo wa 2022/2023 umekuwa ni nyenzo muhimu ya kurahisisha na kuharakisha usambazaji wa mbolea kwa wakulima pamoja na kuzuia mianya yote ya udanganyifu tofauti na ilivyokuwa huko nyuma.

Maadhimisho Siku ya Mbolea Duniani 2022: Wakulima wajengewa uwezo kuhusu matumizi sahihi ya mbolea, kanuni bora za kilimo



Mkuu wa Mkoa wa Rukwa Queen Sendiga akizungumza na hadhira iliohudhuria hafla ya maadhimisho ya Siku ya Mbolea Duniani yaliyofanyika katika viwanja vya Kimondo- Vyvawa Mkoani Songwe tarehe 13 Oktoba, 2022.

Na MATILDA KASANGA na NURU MWASAMPETA

Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) ni chombo pekee kinachosimamia na kudhibiti ubora wa mbolea nchini, Kudhibiti uzalishaji, uingizaji na biashara ya mbolea nchini, kutoa ushauri wa kitaalam kwa Serikali na taasisi nyingine juu ya masuala yanayohusu sera za usimamizi na udhibiti wa ubora na biashara ya mbolea na kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kuelimisha umma juu ya matumizi sahihi ya mbolea.

Lengo la Siku ya Mbolea Duniani

Maadhimisho ya Siku ya Mbolea Duniani, hufanyika mwezi Oktoba 13 kila mwaka duniani kote ambapo kwa Tanzania Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) kama msimamizi mkuu wa tasnia ya mbolea nchini imepewa dhamana ya kuratibu maadhimisho hayo ambayo

Siku ya Mbolea Duniani ilianzishwa ikiwa ni kumbukizi ya uvumbuzi wa mbolea aina ya Amonia uliofanywa na Bw. Fritz Haber mwaka 1908, uvumbuzi uliochochea mapinduzi ya kijani kwa karne ya 20 na kusaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza janga la njaa katika nchi nyingi duniani

kwa mwaka 2022 yaliyofanyika katika viwanja vya Kimondo, Wilaya ya Mbozi, Mkoani Songwe.

Akizungumza kwa nyakati tofauti na wana-habari walioshiriki maadhimisho hayo, Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA, Dkt. Stephan Ngailo anasema, lengo la kuadhimisha Siku ya Mbolea Duniani kwa mwaka 2022 ni kuwaleta pamoja wadau wa mbolea ambapo wadau wapatao 31 wameweza kuonesha bidhaa zao za mnyororo wa thamani katika sekta ya kilimo.

Anawataja wadau hao kuwa ni pamoja na wakulima, makampuni ya mbolea, wazalishaji wa mbolea, wasindikaji wa mazao, taasisi za Utafiti wa kilimo, vyuo vya elimu ya juu, taasisi za serikali na za kiraia.

Katika hotuba, Mkurugenzi Dkt. Ngailo anasema Siku ya Mbolea ilianzishwa ikiwa ni kumbukizi ya uvumbuzi wa mbolea aina ya Amonia uliofanywa na Bw. Fritz Haber mwaka 1908, uvumbuzi uliochochea mapinduzi ya kijani kwa karne ya 20 na kusaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza janga la njaa katika nchi nyingi duniani. Ameongeza siku ya mbolea duniani inafanyika katika juma moja na siku ya chakula duniani ambayo pia inasisitiza uwepo wa chakula bora na cha kutosha kwa kila mtu.

Kauli mbiu

Ikizingatiwa kuwa, Serikali ipo katika kampeni ya utekelezaji wa vitendo wa mapinduzi katika Sekta ya Kilimo ili kufikia azma ya Ajenda 10/30 ya Kilimo ni Biashara inayotoa dira ya kuhakikisha kilimo kinakua kwa asilimia 10 ifikapo mwaka 2030 na hivyo kuongeza mchango wa sekta hiyo kwenye pato la taifa, serikali ime-tenga kiasi cha shilingi za kitanzania bilioni 150 ili kugharamia mbolea za ruzuku kwa wakulima ili kuwawezesha kulima kwa tija na hivyo kuimarisha usalama wa chakula nchini na kuongeza pato la taifa kutokana na tasnia a mbolea.

Akizungumzia umuhimu wa kutumia mbolea kwenye uzalishaji, Dkt. Ngailo anasema, idadi ya watu duniani inatarajiwa kufikia bilioni 9.7 kufikia mwaka 2050. Anasema kuwa, kuongezeka kwa idadi ya watu na maendeleo ya uchumi wa viwanda kutasababisha uhitaji wa kuzalisha mazao mengi kutoka katika eneo dogo. Kwa mfano mwaka 1960 ekari moja iliweza kutoa chakula cha kutosheleza watu wawili (2).

Ameongeza, ifikapo mwaka 2025 ekari itapaswa kulisha watu watano (5). Kutokana na mabadiliko hayo, katika nchi zilizoendelea kama Marekani, baadhi ya maeneo yaliyokuwa yakitumika kwa malengo mengine yamebadilishwa kuwa mashamba ya chakula kutokana na matumizi ya mbolea. Hali hii inaendana na juhudi zinazoendelea hapa nchini kwetu Tanzania za kuhamasisha wakulima kutumia mbolea hususan maeneo yenye udongo usio na rutuba.

>>> **Inaendelea Uk. 12**

Maadhimisho Siku ya Mbolea Duniani 2022: Wakulima wajengewa uwezo kuhusu matumizi sahihi ya mbolea, kanuni bora za kilimo

Kauli mbiu ya maadhimisho ya siku ya mbolea kwa mwaka huu inasema "Agenda 10/30, Matumizi sahihi ya Mbolea ya Ruzuku kwa kilimo chenye tija". Kauli mbiu hii inaendana na jukumu kuu ya TFRA ambalo ni kusimamia ubora wa mbolea ili wakulima wapate mbolea bora na kisha kuongeza tija ya uzalishaji kwa ajili ya kutosheleza mahitaji ya chakula na malighafi za viwanda nchi hii na hata nje ya Tanzania.

Lengo la mbolea ya ruzuku

Naye Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Queen Sendiga anazungumza kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Husein Bashe wakati wa kufunga maadhimisho ya Siku ya Mbolea Duniani anasema, kukua kwa kilimo kunaenda sambamba na ukuaji wa uchumi wa viwanda kwa kuzingatia kwamba viwanda vingi hutegemea malighafi zitokanazo na mazao ya kilimo.

Mkuu wa Mkoa Sendiga anasema, lengo la Serikali la kutoa ruzuku za mbolea ni kupunguza makali ya bei ya mbolea kwa wakulima ili waweze kuongeza uzalishaji na tija katika kilimo, kuimarisha usalama wa chakula nchini na kuongeza mchango wa sekta ya kilimo katika pato la taifa.

Sendiga anaendelea kusema, katika malengo ya muda mrefu, Serikali imeendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza kwenye ujenzi wa viwanda vya kuzalisha mbolea hapa nchini ili kuhakikisha mbolea inapatikana kwa bei rafiki na kwa wakati.

Uzalishaji wa ndani wa mbolea

